**HOTUBA YA MGENI RASMI DKT. BINILITH S. MAHENGE MKUU WA MKOA WA DODOMA KWENYE HALFA YA UZINDUZI WA SOKO LA MADINI MKOA WA DODOMA TAREHE 19 MEI, 2019**

Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini;

Katibu Tawala wa Mkoa;

Wajumbe wa Bodi ya Tume ya Madini;

Viongozi wa CCM Mkoa na Wilaya,

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Dodoma,

Wakuu wa Wilaya;

Makatibu Tawala Wasaidizi Sekretarieti ya Mkoa;

Makatibu Tawala wa Wilaya;

Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wilaya;

Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya;

Wakurugenzi wa Halmashauri;

Watendaji wa Wizara ya Madini na Tume ya Madini;

Viongoziwa Dini;

Wawakilishiwa wachimbaji Madini;

Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Salaam.

Ndugu Wananchi,

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutuwezesha sisi sote kuwa na afya njema na kutuwezesha kusafiri salama hadi mahali hapa na kuwa sehemu ya tukio hili muhimu na lakihistoria la kuzindua Soko la Madini Mkoa wa Dodoma.

Natoa shukurani zangu kwa Washiriki wote mlioitikia kuhudhuria tukio hili muhimu. Uwepo wenu hapa unaonesha utayari wenu wa kuunga mkono azma ya Serikali ya awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. John Pombe Joseph Magufuli zakuendeleza Sekta ya Madini Nchini. Aidha, shukrani za kipekee ziwaendee waandaaji wa hafla hii kwa kunialika kuwa mgeni rasmi. Nichukue fursa hii kutoa pongezi kwa uongozi wa Mkoa wa Dodoma kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Rais ya kuanzisha masoko ya madini hususan katika maeneo yoteyanayochimba madini nchini.

Ndugu Wananchi,

Tangu iingie madarakani, Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikisisitiza dhamira yake ya kuhakikisha Sekta ya Madini inakua, inanufaisha Watanzania pamoja na kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 – 2020 ambayo inaitaka Serikali kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi itakayowezesha kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya utoroshaji madini na biashara haramu ya madini nchini.

Ndugu Wananchi,

Kwa kuzingatia hilo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutoa kipaumbele katika kulinda rasilimali za madini na kuhakikisha zinawanufaisha Watanzania. Juhudi zilizofanyika ni pamoja na kutungwa kwa Sheria Namba 5 ya Mwaka 2017 iliyohusu umiliki wa Maliasili; Mapitio ya Sheria Namba 6 ya Mwaka 2017 yaliyohusu majadiliano kuhusu Masharti hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi na marekebisho ya Sheria ya Madini Sura 123.

Aidha, Serikali imefuta baadhi ya tozo ambazo zilikuwa kero kwa wafanyabiashara ya madini hususani wachimbaji wadogo. Miongoni mwa tozo ambazo tayari zimefutwa ni Kodiya Ongezeko la Thamani (VAT) asilimia 18 na Kodi ya Zuio (*withholdingtax*) ya asilimia 5 kwa Wachimbaji Wadogo.

Ndugu Wananchi,

Serikali inatarajia kuwa kufutwa kwa kodi na tozo hizo kutapunguza utoroshwaji wa madini; kutasaidia wachimbaji wadogo kutambuliwa kupitia uanzishwaji wa masoko ya madini; kupunguza gharama za uendeshaji washughuli za wachimbaji wadogo na kuongeza wigo wa mapato kwa nchi. Nitoe wito kwa wachimbaji wote wadogo kwamba endeleeni kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali katika kutekeleza majukumu yenu kwa kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewana Serikali.

Ndugu Wananchi,

Serikali inachukua hatua zote hizo si kwa lengo jingine bali kuziba mianya ambayo imekuwa chanzo cha utoroshwaji wa madini, ukwepaji kodi, na hivyo, kusababisha biashara nzima ya madini kufanyika kiholela katika maeneo mengi ya nchi yetu. Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali imejipanga vema katika kuhakikisha vikwazo vyote vilivyomo katikamnyororo wa biashara ya madini vinaondolewa kwa lengo la kukuza sekta hii na kuwanufaisha Watanzania mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Ndugu Wananchi,

Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na madini ya aina mbalimbali ambayo ni Dhahabu, Shaba, Nickel, Vito (Chrysoprase, Moonstone, Sunstone,Quartz/Quartzite na Ruby), madini ujenzi (Mchanga, Mawe, Vifusi na Kokoto) na madini yanayotumika viwandani (Jasi, Chuma, Soapstone,Feldspar na Calcite). Shughuli za uchimbaji madini ziliongezeka katika miaka ya 2003 kutokana na ongezeko la waombaji wengi wa leseni za uchimbaji wa dhahabu kwa Halmashauri za Kondoa, Chemba, Chamwinona Bahi na Vito kwa Halmashauri za Mpwapwa, Kongwa na Chamwino.Wastani wa uzalishaji wa dhahabu kwa mwezi ni zaidi ya kilo tatu (3) kwa

Wachimbaji Wadogo. Kutokana na wingi wa shughuli za madini katika Mkoa wa Dodoma na mchango wake kwenye pato la Taifa, Serikali imeamua kuanzisha soko hili tunalolizindua hii leo.

Ndugu Wananchi,

Uanzishwaji wa Soko la madini unatarajiwa kutoa manufaa yafuatayo;

**Mosi**, kuwakutanisha Wachimbaji na Wafanyabiashara kwa lengo la kuuza na kununua madini hivyo kuwapatia wachimbaji wadogo soko la uhakika la madini wanayochimba.

**Pili**, kupitia masoko haya, Serikali inataraji wachimbaji wadogo watapata bei nzuri ya madini kutokana na uwepo wa wanunuzi wa uhakika kutoka ndani na nje ya nchi. Aidha, Tume ya madini itaratibu bei ya madini kwenye soko na kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata mapato wanayostahiki.

**Tatu**, Kuondoa tatizo la kupunjwa na kudhulumiwa kwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa madini wasiokuwa waaminifu. Udhibiti huo utafanyika kwa kuhakikisha vifaa vya kupimia uzito na ubora wa madini vinakuwepo na kutumika ipasavyo kwenye soko.

**Nne**, soko hili pia litaondoa uwezekano wa wanunuzi wa madini kuibiwa na wajanja wachache wanaojifanya kuwa na madini wakati hawana.

**Tano**, Kuokoa muda na gharama nyingine katika kuendesha biashara ya madini kwa kuhakikisha huduma zote muhimu kwenye eneo moja (*onestop center*) kwa wafanyabiashara ikiwemo huduma za Tume ya Madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Halmashauri na nyinginezo.

**Mwisho**, Kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na upatikanaji watakwimu za biashara ya madini.

Ndugu Wananchi,

Ni matumaini yangu kuwa soko hili litakuwa na tija kubwa hivyo tunawajibu wa kuhakikisha kuwa Soko hili linastawi na kuwanufaisha walengwa.

Ndugu Wananchi,

Katika kuhakikisha soko hili linafikia malengo ya kuanzishwa kwake, tunaiomba Wizara ya Madini ishiriki kwenye maeneo yafuatayo:-

**Moja**, Ishirikiane kwa karibu na Serikali ya Mkoa, kusimamia soko hili kikamilifu na kwa ufanisi ili lilete manufaa yanayokusudiwa.

**Pili**, Kupitia Tume ya Madini ihakikishe inakamilisha ufungaji wa Miundombinu na vifaa vyote muhimu na uwepo wa rasilimali watu ya kutosha ili soko hili lifanye kazi kwa ufanisi.

**Tatu**, Iendelee kushirikiana na wadau wote muhimu kuandaa utaratibu maalum wa kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu namna soko linavyofanya kazi, faida zake na mambo mengine yatakayolitangaza soko hili kwa Mchimbaji na Mfanyabiashara na hivyo kulitumia soko ipasavyo.

**Nne**, Ihakikishe Viongozi na Watendaji wote wa Serikali wanasimamia kwa weledi, uaminifu na uadilifu, Sheria, Kanuni na miongozo ya Serikali kuhusu sekta hii ya madini kwa lengo la kudhibiti utoroshwaji wa madini.

**Tano**, Watendaji wa Idara na Taasisi zote za Serikali zinazohusika na Sekta ya Madini kuhakikisha wanaheshimu mipaka ya majukumu yao ili kulisimamia vizuri soko hili na kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

**Sita**, Kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Wachimbaji na Wafanyabiashara wa madini kuandaa Mpango Kazi mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya soko hili ili lisigeuke kuwa kikwazo kipya kwa Wachimbaji na Wafanyabishara wa madini.

**Saba**, Vyombo vya Ulinzi na Usalama tutahakikisha vinatoa ulinzi wa soko wa kutosha katika soko hili muda wote, ili watendaji, mali zitakazokuwemo, vitendea kazi na miundombinu yote iwe salama muda wote.

**Nane**, Kuhakikisha maombi ya leseni za biashara na uchenjuaji wa madini ambayo hayajapatiwa leseni yanakidhi vigezo na kupatiwa leseni hizo kwa wakati ili kila mdau anayehusika na biashara kwenye soko hili atambulike kisheria.

Ndugu Wananchi,

Kufuatia kuanzishwa kwa masoko haya niwasihi wadau wote wa madini kulitumia soko hili na kuacha vitendo vya utoroshaji wa madini. Serikali kwa upande wake, haitomvumilia mtu yeyote yule atakaye jihusisha na utoroshaji wa madini. Nitoe tahadhari kwa wadau wote wa madini kuwa atakayekamatwa anatorosha madini, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo utaifishaji wa madini atakayokuwa akiyatorosha.

Ndugu Wananchi,

Kama mtakavyoona, lengo la Serikali kuanzisha masoko ya madini ni zuri na lina maslahi mapana ya nchi. Hivyo, ni vyema tuhakikishe kwa pamoja tunayalinda masoko haya, tunayatetea na tunayawezesha kwa kadri tunavyoweza. Kwa upande wa Serikali, itahakikisha masoko haya yanaendeshwa kwa njia shirikishi, uwazi na uadilifu ili sote kwa pamoja tunufaike nayo.

Mwisho, nimalizie kwa kuwashukuru wote kwa kufika kwenye shughuli hii muhimu, na kwa kuunga mkono jitihada hizi ambazo Mheshimiwa Rais wetu amezipigania na hatimaye leo tumezindua Soko la madini katika Mkoa wetu wa Dodoma. Wote Hongereni sana.

Ndugu Wananchi,

Baada ya kusema hayo, sasa nipo tayari kuzindua rasmi Soko la Madini Dodoma.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**